# MCHANGO WA DINI YA KIISLAMU KATIKA KUJENGA UTANGAMANO WA KIMBARI KATIKA JAMII YA ZANZIBAR: MIFANO KUTOKA KATIKA RIWAYA YA *VUTA N'KUVUTE*

*Ulfat Abdulaziz Ibrahim*
*Chuo Kikuu cha SUMAIT , Zanzibar - Tanzania*
*madamullu@gmail.com*

*Mohamed Omary Maguo*
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania – Tanzania*
*omarymohamed36@gmail.com*

## Ikisiri

*Imani ya dini ni kitu chenye nguvu sana katika maisha ya mwanadamu. Shafi Adam Shafi analithibitisha jambo hili kupitia riwaya yake ya Vuta N'kuvute (1999) pale ambapo kuna vikwazo, miiko na desturi ya kutoingiliana kindoa au kimapenzi kwa jamii au mbari tofauti, bado imani ya dini inaweza kuvunja mipaka hiyo. Jamii ya Zanzibar ni yenye mseto wa Waislamu wenye asili mbalimbali kama vile ya Kiarabu, Kihindi na Kiafrika. Maingiliano ya kindoa baina ya Waarabu na Waafrika au Wahindi na Waafrika yamekuwa yakitokea kwa nadra na vikwazo tangu kipindi cha karne ya 18. Jamii ya Waasia Waislamu inayogawanyika katika mbari kama vile za Mashia Ithnasheri, Mashia Bohora, na Suni wa Gujarati na Punjabi nao hupendelea kujitenga na kutoruhusu mahusiano ya kindoa hususani na Waislamu wenzao ambao ni Waafrika. Shafi Adam anavunja mwiko huo kupitia mhusika Yasmin ambaye ni Mhindi. Mhusika huyu anakuwa na mahusino ya kimapenzi na mbari nyingine ambazo kwao ni mwiko kutangamana nazo. Licha ya tofauti ya mbari zao, wanaungana kutokana na imani yao ya dini ya Uislamu. Dini ya Kiislamu inakuwa ni sababu ya kuleta utangamano na kujenga jamii mpya isiyo ya kibaguzi. Utafiti huu mdogo ni sehemu ya utafiti mkubwa ambao ulilenga kuchunguza migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya baada ya ukoloni. Mbinu zilizotumika kukusanyia data ni usomaji makini na uchambuzi matini. Makala hii imelenga kubainisha jinsi imani ya Uislamu inavyosaidia kujenga utangamano wa mbari tofauti na kuvunja mila potofu zilizojengeka katika jamii, hususani Zanzibar. Kupitia riwaya ya Vuta N'kuvute, utafiti umebaini dini ya Kiislamu imetoa mchango mkubwa katika kujenga utangamano wa kimbari katika jamii. Jamii mpya inazaliwa kutokana na kuacha kutii mila potofu zinazojenga ubaguzi. Wanajamii wanatumia fursa ya dini katika kuijenga Zanzibar mpya.*

## 1.0 Utangulizi

Riwaya ya *Vuta N'kuvute* inahusu maisha ya msichana wa Kihindi wa madhehebu ya Kiislamu ya Kishiaithnashiri aliyelazimishwa kuolewa na mume mzee lakini wa ukoo wake. Ndoa yenye baraka za wazazi wake, ndugu na jumuiya ya Jamatkhan ya Shia Ithnashir. Akiwa ni msichana mdogo, hakupendezwa na kulazimishwa kuingia katika ndoa hiyo na Bwana Raza. Aliyachukulia maisha ya kulazimishwa katika ndoa kuwa ni sawa na ufungwa. Hivyo, aliamua kutoroka huko Mombasa na kurudi Zanzibar ambapo jamii yake inamkataa na kumfukuza. Anafadhiliwa na rafiki yake, Mwafrika, na anaaanza kuishi maisha ya Uswahilini. Katika maisha yake ya Uswahilini, anajifunza mengi yanayokuwa sehemu ya maisha yake. Anaingia katika mahusiano ya kimapenzi na mbari[1] mbalimbali, akiwamo Mwafrika aitwaye Denge, na anavunja miiko yote ya kutangamana na Waafrika. Katika mwendelezo wa riwaya hii, inagundulika kuwa mjomba wake Yasmin naye alioa mke wa pili ambaye ni Mwafrika na kuzaa naye. Haya ni mabadiliko ambayo mwandishi ameyaibua yaliyoikumba mbari ya Kihindi.

Ndoa ya Yasmin na wanaume kutoka mbari tofauti inathibitisha kuondoka kwa "U-golo" na "Uponjoro" (uk. 245) kunakoashiria suluhisho la utangamano wa kimbari. Mandhari za Unguja, Mombasa na Tanga zinahusishwa na mwandishi katika suluhisho la migongano ya kimbari. Yasmin anaamua kuachana na mila zao za kibaguzi kwa kumkataa mume wa Kihindi aliyeozeshwa na wazazi wake. Kwa vile Yasmin alikuwa Muislamu, aliitumia fursa hiyo inayomruhusu kuolewa na mbari yoyote. Uthibitisho kuwa Yasmin alikuwa Muislamu ni madhehebu yake ambayo ni Shia Ithnashir. Mwandishi anataja sehemu ambayo waumini wa Shia Ithnashiri hukusanyika kwa ajili ya ibada, nayo huitwa Jamatini. Yasmin alipokwenda kwa mjomba wake, alimuuliza mke wa mjomba wake kuwa "mjomba yuko wapi?", naye alijibiwa kuwa yuko Jamatini (uk. 15). Vilevile, mwandishi anabainisha kuwa Yasmin anatoka katika madhehebu ya Kiislamu ya Shia Ithnashir wakati mama yake Yasmin anamgombeza mwanawe juu ya aliyoyafanya anasema, "Jamatini vatu ote nazungumza habari yako" (uk. 38). Hii inadhihirisha kuwa Yasmin ni miongoni mwa wanaokutana Jamatini. Ushahidi mwingine tunaupata kwa Yasmin wakati alipofiwa na mume wake, Shihab. Mwandishi anasema kuwa Yasmin

---

[1] Mbari ni jamii ya watu wa kitovu kimoja; ukoo, kabila au jamii yenye utamaduni mahususi (TUKI, 1981: 229).

lazima aende Tanga akakae eda (uk.194). Ibada ya eda hufanywa na Waislamu.

Uislamu ni dini kubwa visiwani Zanzibar. Kwa mujibu wa makala iliyochapishwa na gazeti la *An-nnur* mnamo tarehe 2-8 Oktoba mwaka 1998, Uislamu uliingia Zanzibar tangu karne ya 10. Ushahidi wa hilo ni mabaki ya misikiti yaliyogunduliwa katika miji ya kale katika visiwa vya Zanzibar kama vile Unguja Ukuu, Kaepwani (Mkoa wa Kusini Unguja) na Mtambwe Mkuu (Mkoa wa Kusini Pemba). Makala hiyo inaeleza sababu ya kuibuka kwa Uislamu kuwa ni biashara kubwa baina ya miji hii ya kale ya visiwa vya Zanzibar na miji muhimu ya Kiislamu ya wakati huo katika nchi za Kiarabu kama vile Iraki na Misri. Mnamo karne ya 11, wakimbizi na wafanyabiashara waliendelea kufika mwambao wa pwani. Wengine walioa na baadhi waliamua kuishi moja kwa moja katika miji ya Waswahili.

Pamoja na kutangulia kuwapo kwa Uislamu ambao ulileta na Waarabu, suala la migongano ya kimbari kwa wakati huo halikuwapo. Kama historia inavyoeleza, watawala wa kigeni waliotawala Zanzibar ndio wamesababisha utabaka na hatimaye kuzuka migongano ya kitabaka na kimbari. Migongano ya kimbari imeota mizizi katika ngazi za kijamii mpaka kuwekeana vikwazo katika mahusiano. Hili si jambo geni kwa jamii zilizopitia utawala wa kigeni kama anavyoeleza Bhabha (1994) kuwa hali ya ubaguzi wa kichotara na kimbari ni sifa mojawapo ya jamii za ubaadaukoloni.

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhimiza usawa na utambulisho wa Wazanzibari bila kujali asili za mabibi na mababu zao, jamii ya Zanzibar inaibuliwa kama jukwaa ambalo suala la ndoa na maingiliano ya kimapenzi baina ya wanajamii wa mbari tofauti limekuwa halikwepeki.

Kwa kushadidia hoja hiyo, Ricard (2000) anasema katika visiwa vya Zanzibar, jamii ya Kihindi imekuwa katikati ya mgongano huo ulioasisiwa tangu mwaka 1840 na Sultani wa Zanzibar na Omani alipochukua hatamu za utawala wa taifa la Zanzibar na kuwakaribisha Wahindi katika nafasi na fursa za uongozi na biashara.

Makala hii inakusudia kuangazia nafasi ya imani ya kidini, hususani Uislamu, inavyosaidia kuleta utangamano katika jamii ya Zanzibar. Makala inafafanua namna mwandishi Shafi Adam Shafi anavyowasawiri wahusika wake kama wapigania haki ya kuvunja mwiko wa ndoa na mahusiano ya kidamu baina ya mbari za Kihindi na Kiafrika katika jamii yake, na kusimamia imani ya dini yao (Uislamu) ambayo inawaruhusu kujenga utangamano na mbari yoyote.

## 2.0 Umbari katika Jamii ya Zanzibar

Chimbuko la makutano ya mbari tofauti katika Zanzibar yanatokana na ukoloni katika visiwa hivyo. Mwaka 1821, Sultani Seyyid Said aliwakodisha Wabaluchi (Mabulushi), Washihiri, Wahindi, Waturuki, na Washirazi kuja visiwani Zanzibar pamoja na sehemu za pwani za Afrika ya Mashariki. Kutokana na umuhimu wa Zanzibar kama kitovu cha biashara, Sultani Seyyid Said, aliyekuwa mtawala wa Omani na Zanzibar, aliamua kuhamishia makao yake makuu Zanzibar ili kuimarisha biashara yake mwaka 1840 (Sherrif, 1987; Chachage, 1996).

Kipindi hicho cha Sultani Seyyid Said kilifanikiwa kujenga himaya kubwa yenye nguvu ambapo aliwakaribisha Wahindi na Waarabu kushiriki katika kilimo cha karafuu na minazi. Sultani Seyyid Said alipitisha sheria ya kumilikisha ardhi yenye rutuba kwa wafuasi wake wa Kiomani na Washirazi kwa ajili ya kilimo cha mikarafuu na minazi. Wahindi pia walimsadia katika kuendesha kilimo cha kibiashara hasa katika kutoza ushuru wa forodha na kutoa mitaji ya biashara ya watumwa na pembe za ndovu kwa waliokuwa wanakwenda bara (Sherrif, 1987).

Kwa kuwa Zanzibar ilikuwa kitovu cha biashara, bandari yake ilitembelewa na meli za Kidachi, Kiingereza na hata za Kifaransa. Jamii ya Zanzibar ilipokea wageni kutoka maeneo mbalimbali waliokuja kwa ajili kufanya biashara. Hatimaye, wakoloni nao wakapata nafasi ya kuingia Zanzibar.

Mwaka 1873, jeshi la Uingereza lilimlazimisha Sultani Barghash kukubali kusitishwa kwa biashara ya utumwa mwaka 1885. Vilevile, Sultani Barghash alilazimishwa na Wajerumani kuachia madaraka ya utawala wake wa sehemu za bara (Tanganyika). Kwa upande wa Zanzibar, visiwa hivyo vilikuwa chini ya himaya ya utawala wa Kiingereza. Mwaka 1963, serikali ya kikoloni ya Kiingereza iliendesha uchaguzi mkuu wa kwanza

wa vyama vingi na ushindi ulienda kwa vyama vya ZPPP na ZNP ambavyo vilikuwa na mrengo wa kisultani. Haukupita muda mrefu, serikali hiyo ilipinduliwa na Waafrika walio wengi chini ya chama cha ASP mnamo mwaka 1964 (Lofchie, 1965; Sheriff 2001).

Mfumo wa kikoloni wa Kiingereza na kisultani ulijenga matabaka na mgawanyo wa kiutamaduni hususani kati ya Wahindi, Waarabu na Waafrika. Tabaka la wafanyabiashara, hasa wa Kihindi, lilijitenga dhidi ya Waafrika katika utangamano wa damu kiasi cha kuendelea kuwa wageni (Fouéré, 2015). Shafi anathibitisha hayo pale anapolizungumzia tabaka hilo:

> Kama desturi ya Wahindi wengi Afrika ya Mashariki, Bwana Raza alikuwa mfanyabiashara mashuhuri pale Mtendeni (uk. 1).

Vilevile, waandishi Topan (1971) na wa Thiong'o (1977) nao wanathibitisha kuwa jamii ya Kihindi imejipambanua kuwa ni jamii ya wafanyabiashara kupitia wahusika Salimu, Abdulla na Bwana Raza katika kazi zao za *Mfalme Juha* na *Petals of Blood*, wakiwa sehemu ya mfumo ulioasisiwa na wakoloni.

Athari hizi za kisultani na kikoloni zimeifanya Zanzibar kuwa na mbari mbalimbali. Wanajamii ya Zanzibar wamegawika kutokana na asili zao, na kufuata mila na tamaduni za asili hizo. Mathalani, Wazanzibari wenye asili ya Uhindi waliendeleza mila potofu za kibaguzi. Waafrika walionekana kuwa ni watu wa tabaka la chini. Kama anavyoeleza Frouéré (2015) kuwa Waafrika walio wengi walikuwa ni wafanyakazi wa kazi za mitulinga, kama ilivyo katika riwaya ya *Kuli*. Jambo hili limegusiwa na waandishi wengi wa kazi za fasihi wa Zanzibar, kama vile Mohammed (1978), Mohammed (1989, 2007), Shafi (1979, 1999) na Bahroon (2017).

Waandishi wa kazi za fasihi kutoka Zanzibar hawakuacha kulizungumzia suala hili la migogoro inayosababishwa na umbari. Hoja hii inaungwa mkono na mhakiki Traore (2012) alivyoyaibua masuala ya migogoro ya kimbari kupitia riwaya za *Dunia Mti Mkavu (2007), Asali Chungu (1989)* na *Nyota ya Rehema (1978)*. Ubaguzi ulivuka mipaka ya makazi na koo na kuingia katika miiko ya kuoleana na kuzaa machotara. Mfumo wa ndoa ya kiudugu ndio uliopendelewa na kustawishwa miongoni mwa

jamii ya Wahindi wa Zanzibar. Sababu kuu ya jamii ya Kihindi kukataza ndoa au mahusiano ya kimapenzi na Waafrika au jamii nyingine ni kwamba wanajihesabu kuwa wao wapo katika tabaka la juu ambalo limewekwa na wakoloni wa Kiingereza na utawala wa kisultani ambapo tabaka la Wazungu, Waarabu na Wahindi lipo juu ya Waafrika.

Kwa muhtasari, mwandishi ameelezea jamii ya Zanzibar ilivyo na mseto wa mbari mbalimbali na namna mbari hizo zinavyowaingiza wanajamii katika migongano. Aidha, kwa muktadha wa makala hii, mwandishi anazungumzia zaidi mbari ya Kihindi katika visiwa vya Zanzibar. Jamii ya kimbari ya Kihindi ikiwa katikati ya mgongano huo ulioasisiwa tangu mwaka 1840 na Sultani wa Zanzibar na Omani alipochukua hatamu za utawala wa taifa la Zanzibar na kuwakaribisha Wahindi katika nafasi na fursa za uongozi na biashara (Ricard, 2000).

Vilevile, mbari ya Kihindi ndiyo jamii ambayo mwandishi Shafi (1999) ameisawiri katika riwaya yake ya *Vuta N'kuvute* kwa kumtumilia mhusika wa Kihindi aitwaye Yasmin. Alipoulizwa na Lutz Diegner (2009) kwa nini amemteua mhusika mwanamke mwenye asili ya Kihindi kama mhusika mkuu katika riwaya yake ya *Vuta N'kuvute*, mwandishi Shafi Adam Shafi alijibu:

> Nimemchagua Muhindi kuonyesha kama mhusika mkuu kwa kutaka kuondoa ile imani kwamba Wahindi ni watu tafauti na Waswahili, au Waswahili ni watu tafauti na Wahindi. ... Na ndiyo mpaka mwisho utaona kwamba Yasmin anaolewa, inafanywa sherehe, katika ile sherehe wanachanganyika wote, wazazi wake Yasmin, na wazazi wake Bukheti, Wahindi na Waswahili, wanasherehekea, hakuna tena 'Golo', hakuna tena 'Ponjoro'. Sasa nimechukua hii ili ... nilitaka kuonyesha uhusiano mzuri wa makabila kwamba unawezekana.

## 3.0 Imani ya Dini (Uislamu) na Utangamano katika Jamii

Mapenzi na ndoa ya Kiislamu yavunja ubaguzi wa kimbari. Ndoa ni makubaliano baina ya mwanamke na mwanamume, kwamba wapo tayari kuishi pamoja na kuanzisha familia ambapo mmoja atakuwa mama na mwingine atakuwa baba katika familia hiyo iliyoanzishwa (Mlacha, 1996).

Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, mwandishi amemsawiri mhusika Yasmin kuwa ni kivutio cha wanaume wa mbari zote – Wahindi, Waafrika na machotara. Kama ua la asumini, hunukia kwa yeyote yule mwenye pua na uwezo wa kutambua harufu nzuri. Yasmin anaolewa na Mhindi, chotara na Mgunya katika ndoa ya Kiislamu. Ndoa ya kwanza ni ya mume ambaye anatokana na jamii yake ambaye alilazimishwa na wazee wake. Wazee wa Yasmin walifanya maamuzi ya kumlazimisha mtoto wao aolewe na mume ambaye hakumpenda. Mzee Raza kwa Yasmin alikuwa kama babu yake kwa umri; hata hivyo, wazee wa Yasmin walimlazimisha Yasmin hata kama hakuwa tayari kuolewa. Mwandishi anaelezea jambo hili kama ifuatavyo:

> Mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasimini aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya Ithinaashiria ambaye alikuwa akiishi jirani naye hapo Mtendeni. Alikuwa ni mume asiyelingana naye hata kidogo. Si kwa umri wala tabia, kwani wakati Yasmin ni kigoli wa miaka kumi na tano tu, mumewe bwana Raza alikuwa zee la miaka hamsini na mbili. Wakati bwana Raza keshazeeka, Yasmin alikuwa mtoto mbichi asiyeelewa kitu chochote. Kukubali kwake kuolewa ilikuwa ni kwa sababu ya kuwaridhi wazee wake tu. Yeye mwenyewe hakuona fahari ya kuolewa na mzee anayeweza kumzaa. Hakupenda kufuatana na mumewe pahala popote na hata ile siku inayotokea wakaenda senema, basi yeye hapendi kukaa karibu naye (uk. 1).

Dondoo hii linaonesha kuwa Yasmin aliozwa kwa mwanamume ambaye alitokana na mbari yake. Jambo hili liliwafanya wazazi wake wafurahi sana kuona likitokea katika maisha ya mtoto wao mpendwa, ingawa yeye binafsi hakupenda kuona suala la kuolewa na mzee likitokea katika maisha yake. Wazee wa Yasmin hawakuzingatia umri wala mapenzi ya wanandoa hawa wawili. Wao walipoona binti yao ameshavunja ungo, wakaamua kumuoza kwa sababu ndoa katika jamii ni jambo jema na la heshima. Jambo hili katika jamii si geni kama anavyoeleza Adam *(keshatajwa)*, kutokana na umuhimu wa ndoa. Kama ilivyoonekana katika jamii, baadhi ya watoto wa kike waliozwa wakiwa wadogo tu, tena pasipo ridhaa yao. Maadamu wazazi wamekwisha kuamua, mtoto hawezi kupinga hata kama hakupenda kitendo hicho.

Mume wa pili wa Yasmin ni mume ambaye alikuwa chotara, aliyeishi Tanga, akijulikana kwa jina la Shihab. Shihab alimpenda sana Yasmin, ila wivu uliopitiliza ulimfanya Yasmin ajione kama yuko gerezani licha ya kupata kila starehe. Mwandishi anaeleza kama ifuatavyo:

> Alimpa kila starehe, ila uhuru wa kutoka na starehe zake zote ziliishia ndani ya nyumba yake kubwa iliyokuwa na kila aina ya anasa ndani yake, zote asizione kitu, kutwa akawa ananing'inia madirishani akiangalia wapitao njia na kuwahusudu jinsi walivyo huru (uk. 197).

Baada ya muda, Shihab alifariki dunia kutokana na mshtuko wa moyo baada ya kupata taarifa ya kwamba ndege aliyopanda mke wake (Yasmin) imeanguka. Ingawa Yasmin hakuwamo kwenye ndege hiyo. Shihab hakulijua hilo. Mwandishi anamuelezea Yasmin alivyokuwa na majonzi ya kufiwa na mume wake, akisema, "aliruka pale alipokuwa amekaa akamkumbatia Denge, kichwa chake amekilaza juu ya bega la Denge, akilia na kulalamika, 'Mume wangu masikini Shihab " (uk. 194).

Baada ya msiba huo, mwandishi alisawiri muktadha wa Yasmin kukaa eda kama sheria ya dini ya Uislamu inavyomtaka. Eda ni kipindi maalumu anachokaa mwanamke aliyeachika au aliyefiwa na mumewe, na baada ya kipindi hicho, mwanamke huyu anayo nafasi ya kuolewa na mume mwingine. Ushahidi wa jambo hili unatokana na maamrisho ya kitabu cha

Quran kinachosema, "...na wale wanaokufa miongoni mwenu na kuacha wake; hawa wake wasubiri (wasiolewe) miezi minne na siku kumi" (2:234) (Tafsiri ya Sheikh Ali Muhsin Al-Barwan).

Kipindi hiki cha miezi minne na siku kumi ndicho hujulikana kwa jina la eda. Kwa vile ibada hii hufanywa na Waislamu mwandishi amesawiri muktadha wa kufanyika ibada hii kwa Yasmin. Shafi analidhihirisha hili kwa kusema, "Msiba umempata Yasmin. Sasa lazima afunge safari ya Tanga akamkalie eda mumewe" (uk. 194).

Kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu, mwanamke akimaliza kipindi hiki cha eda, basi yuko huru kuolewa. Naye Yasmin alipomaliza eda ya mume wake, Shihab, alifunga tena ndoa ya tatu.

Yasmin alifunga ndoa ya tatu na Bukheti ambaye ni Mgunya atokaye Mombasa. Bukheti alikuwa akiishi Mombasa. Kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo kwa Yasmin, alisafiri kwenda Zanzibar kwenda kumtafuta Yasmin. Katika riwaya hii ya *Vuta N'kuvute*, mwandishi anathibitisha hilo kwa kusema:

> Bukheti alisikia redioni yakamrusha roho. Akahisi Yasmin hana bahati ya ndoa… nafikiri iliyoandikwa ni yangu mimi na yeye (Bukheti alisema). Bukheti akaifunga tena safari ya Unguja (uk. 196).

Yasmin alipokutana na Bukheti, akaufungua moyo wake na kukubali kuolewa na Bukheti. Kupitia mwandishi, Yasmin anasema, "Sikiliza Bukheti, posa nimeikubali lakini lazima uipeleke posa hiyo kwa wazazi wangu kwa desturi zinazotakiwa" (uk. 206). Bukheti aliweza kukamilisha masharti aliyopewa na hatimaye ndoa ikafungwa, kama anavyoeleza mwandishi, "Bukheti alihamia Unguja… harusi yake na Yasmin ilikuwa ni ya kukata na shoka" (uk. 245).

Kama inavyothibitika katika riwaya hii ya *Vuta N'kuvute*, Yasmin ameolewa mara tatu na waume wa mbari tofauti. Licha ya kwamba jamii yake ya Kihindi haipendelei utangamano wa kijamii na mbari nyingine,

imani yake ya dini (Uislamu) imempa nafasi ya kuolewa na yeyote ampendaye.
Kwa upande mwingine, mjomba wake Yasmin, aitwaye Gulam, anatumia uhuru wake kama Muislamu kuoa mke wa pili. Mila zao hazikuruhusu kuoa mke kutoka katika mbari nyingine tofauti na ya kwao. Wahindi wanaendeleza mila zao za kuoana wao kwa wao lakini pia kufanya kila jitihada za kusuluhisha migogoro ili familia zisiachane.

Maelezo hayo yanaungwa mkono na Adam (2014) anapoelezea juu ya suala la ndoa katika mbari ya Kihindi. Anasema kuwa utaratibu wa ndoa za kiudugu, hususani kwa Wahindi wa madhehebu ya Kishia, hupendelewa kama mkakati wao wa kuendeleza mshikamano wa kifamilia. Suala la talaka ni gumu kutokea na maamuzi hufanyika katika Jamaatkhan ambapo suala la umoja ni nguzo kuu ya kuimarisha utambulisho na tabaka lao.

Ujasiri wa Gulam wa kuoa mke wa pili kutoka mbari tofauti na ya kwake unasababishwa na imani yake ya dini. Uislamu umehalalisha mwanamume kuoa mke zaidi ya mmoja. Mwandishi amebainisha nguvu ya dini dhidi ya mila na desturi za kibaguzi katika kuleta utangamano katika jamii.

Ushahidi wa haya tunaupata katika kitabu kitukufu cha Quran kinachosema "… Oeni mnaowapenda katika wanawake, wawili au watatu au wanne…" (4: 3) (Tafsiri ya Sheikh Ali Muhsin Al-Barwan).

Mzee Gulam aliitumia fursa hii na kutupilia mbali suala la mila. Kwake yeye, nafasi ya dini ni kubwa zaidi na ndiyo inayomruhusu kuoa yeyote anayempenda. Hata hivyo, kwa kuepuka migogoro kwa familia yake, aliamua kufunga ndoa kwa siri ili jamii yake ya Kihindi isijue kwani ni kinyume na mila zao. Haya yanaelezwa katika riwaya hii kama ifuatavyo:

> Anaye mke Mswahili! Tena anaye siku nyingi, amezaa naye watoto wawili wa kiume tena wakubwa sasa. Amemwoa kwa siri. Ni siri hajui mtu yeyote. Yuko Vikokotoni" (uk. 224).

Nukuu hii inathibitisha kuwa kweli Gulam alioa mke wa pili tena kwa siri. Adam (2014) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa suala la jamii ya Wahindi kutaka waoane wao kwa wao linatokana na wao kutaka

kudumisha asili yao. Aliyaeleza haya kutokana na maelezo aliyoyapata baada ya kufanya mahojiano na Bwana Mohamed Ravji ambaye ni Mhindi anayeishi Mkunazini Zanzibar. Alipofanyiwa usaili na Adam (2014), alisema:

> Unajua, bwana mtafiti, watu wengi, hasa Waswahili, wanashindwa kutuelewa sisi vizuri. Sisi hatuwachukii Waswahili, bali sisi tunapenda kudumisha asili yetu iendelee kuwepo duniani. Sidhani kama kuna mtu ambaye anapenda kuipoteza asili yake. Njia pekee na kubwa katika kutimiza hili ni kuhakikisha kwamba, tunaoana sisi kwa sisi ili kuweza kuidumisha asili hii na tusipofanya hivyo basi sisi tutakwisha. Hii ni sera ambayo, ipo kwa Wahindi wote, wanaoishi katika sehemu mbalimbali duniani na si hapa Tanzania peke yake. Kwangu mimi ninamuona Mswahili kuwa ni mwanadamu na anastahiki kupata heshima zote za kibinadamu, lakini mimi nina utamaduni wangu na yeye ana utamaduni wake (uk. 74).

Dondoo hilo limedokeza jambo la msingi kwamba jamii ya Kihindi inashikilia msimamo wa kuoana katika mbari yao pekee kwa sababu ya kudumisha asili yao ili iendelee kuwapo duniani. Hofu yao ni kupotea kwa asili yao tu. Hata hivyo, mabadiliko ya kiulimwengu yanaikumba kila jamii na kufanya mapinduzi dhidi ya mila zao. Sehemu yoyote yenye mchanganyiko wa watu wenye asili tofauti haiwezi kuepuka uchotara. Kama anavyoshadidia Bhabha (1994), uchotara huingilia mfumo jadi uliokuwapo na kuunda mfumo mseto. Mfumo huu mseto unatokana na kizazi kipya kinachotokana na mbari mbili tofauti, mathalani, Dhahir, mtoto wa Yasmin aliyezaa na Denge.

Wahusika wawili hawa (Yasmin na Gulam) walitumia fursa iliyotokana na misingi ya dini yao (Uislamu) na kuachana na hizo tamaduni kama anavyodai bwana Mohamed Ravji. Hii ni kwa sababu, katika Uislamu, hakuna kabila bora zaidi ya jingine aliye bora ni yeyote aliye mchamungu. Tofauti ya kabila ni kwa ajili ya kutambuana kama Kurani inavyosema:

> "Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanaume (mmoja, Adamu) na yule yule) mwanamke (mmoja Hawaa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane (tu basi, siyo mkejeliane). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule ambaye mcha Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote)" (Qura. 49:13) (Tafsiri ya Sheikh Ali Muhsin Al-Barwan).

Aidha, katika Uislam kuna nafasi ya mwanamume kuoa zaidi ya mke mmoja, kama ilivyokwishaelezwa hapo awali. Vilevile, kuna mazingira ya mwanamke kuolewa na mume mwingine baada ya kutengana (kwa kupewa talaka au kufiwa) na mume wake (Kurani 2: 234). Hivyo, katika suala la mapenzi, dini ya Kiislamu haina mipaka ya kimbari, bali inaondoa mipaka ya kimbari.

*Vuta N'kuvute* ni riwaya yenye kuonesha athari na nguvu ya dini dhidi ya mila katika jamii. Itikadi ya Kiislamu kuhusu mapenzi ya ndoa hairuhusu ubaguzi wa aina yoyote. Hii inatokana na kuwa katika dini hakuna kabila bora. Ubora ni wa mja mwenyewe katika kufuata maamrisho ya dini. Yasmin hajali kitendo cha kutengwa kwani anajiunga na Waafrika ambao wanamkubali na kumpenda. Waafrika Wanamsitiri kwa mavazi, malazi na chakula. Anavunja fikra za utengano wa kindoa pale ambapo zimejengeka katika jamii yake na hilo linathibitishwa na Waafrika na Wahindi pia pale ambapo Bukheti anataka kumposa Yasmin ambapo Bukheti anatilia mashaka jambo hilo kwa kusema, "Unafikiri Mhindi atasikiliza posa ya Mgunya atokaye Mombasa?" (uk. 207).

Vilevile, kwa upande wa familia ya Bukheti, kutokana na tamaduni zilizozoeleka, kuwa Mhindi huolewa na Mhindi mwenziwe, wazee wake walikuwa na hofu ya kukataliwa; hivyo, walimshauri kijana wao kuwa ni vyema aoe katika jamaa zake. Wanasema:

> "Ya nini kwenda kutafuta Wahindi mwanangu. Wewe una jamaa zako chungu nzima, kuumeni na kukeni" (uk. 226).

Hali ya uatiati (*inbetweenness*) ya Yasmin imemfanya ajione ni mtu wa mchanganyiko wa Kihindi na Kiafrika, na hawezi kuegemea upande mmoja. Kwa kuitumia taasisi ya ndoa ya Kiislamu, anafanikiwa kulitatua

suala hilo. Mwandishi kupitia mhusika Yasmin anaongoza mapambano kujenga utangamano bila ya kushuritishwa na wanajamii au kwa sera za serikali. Watoto wanaozaliwa ni wa kichotara, ambao ni uthibitisho tosha wa utangamano. Kwa mujibu wa Bhabha (1994), hali hiyo ni matokeo ya kuambatana na kuingiliana mbari tofauti na kuunda uwanda wa tatu na ni nafasi inayozua taifa jipya. Mafunzo aliyoyapata Yasmin wakati akiwa nyumbani kwa Mwajuma yalimfungua macho na kuondokana na tongo za kushikilia mila zao ambazo zilikuwa ni za kibaguzi. Kwa maneno ya Shafi, anampa sifa Yasmin kuwa ni:

> Mfano wa jinsi gani watu wa makabila mbalimbali wanaweza kuwa pamoja, wakawa wamoja hata tofauti baina yao zisionekane" (uk. 75).

## 4.0 Hitimisho

Bhabha (1994) anajenga hoja kuwa utamaduni si jambo lenye kubaki katika hali ileile isiyo ya mabadiliko. Utamaduni ni mchakato wa mabadiliko ambapo hakuna utamaduni wenye hali ya umenyu. Mbari ya Kihindi ina mchanganyiko wa imani mbalimbali ikiwamo ya Kiislamu. Dhehebu la Yasmin na mjomba wake, Gulam ni Shia Ithnasheri, ambalo ni dhehebu la Kiislamu. Linakumbwa na mabadiliko yanayoletwa na Gulam, kwa siri, na Yasmin, kwa dhahiri, kupitia muegamo wa dini ya Kiislamu. Mwiko wa kutokuoleana unavunjwa kivitendo na Yasmin na Gulam. Taasisi ya ndoa ya Kiislamu inalikaribisha tendo la kuoana baina ya mbari tofauti chini ya misingi ya Uislamu. Kufuatia ndoa ya Yasmin na Bukheti na Gulam na mke Mswahili jamii ya Zanzibar inazaliwa upya. Dhambi ya chuki inasafishwa na ndoa yenye baraka za wazazi na ndugu wa pande zote mbili. Yasmin, kama ua, anawanukisha wanajamii harufu nzuri ya manukato ya upendo, amani na maelewano. Kwa Shafi, mapinduzi ya kweli yenye mafanikio na uthabiti ni yale yanayoongozwa na wanyonge, hususani tabaka la wanawake wanaogandamizwa na mfumodume na upofu wa ubaguzi. Vilevile, nguvu ya dini ni kubwa sana katika kuleta suluhisho la migogoro ya muda mrefu.

**Marejeleo**

Al-Barwani, A. M. (2000). *Tarjama ya Al Muntakhab katika Tafsiri ya Quran Tukufu*. Abudhabi: Dar- Al-Fajr Al- Islami Press.

Bahroon, Z. (2017). *Mungu Hakopeshwi*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Bhabha, H. (1994). *The Location of Culture*. New York: Routledge.

Chachage, S. (1996). *Environmental Aid and Politics in Zanzibar*. Dar es Salaam: DUP

Fouéré, M.A. (2015). "Indians are exploiters and Africans idlers!: Identity formation and socio-economic condtions in Tanzania" Katika M. Adam (Ed.), *Indian Africa: Minorities of Indian-Pakistani Origin in Eastern Africa*. 359-396. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Lofchie, M. F. (1965). *Zanzibar: Background to Revolution*. Princeton: University Press.

Mhariri wa Gazeti. (An-nnur 1998, Oktoba, 2-8). Uislamu ulivyoingia Zanzibar. An-nnur, 169.

Mlacha, S.A.K. (1996). Utamaduni wa Mwafrika katika riwaya ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. *Mulika*, *23*, 24-35.

Mohamed, M. S. (1978). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (1989). *Asali Chungu*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (2007). *Dunia Mti Mkavu*.5th Ed, Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Ricard, A. (2000). *Swahili Theatre and Individualism*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Shafi, A. (1979). *Kuli*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Shafi, A. (1999). *Vuta N'kuvute*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Shafi, A. and Diegner, L. (2011). Mazungumzo na Adam Shafi juu ya uandishi wake wa riwaya. *Swahili Forum*. 18, 37-68.

Sheriff, A. (1987). *Slaves, Spices, and Ivory in Zanzibar*. Ohio: Ohio University Press,

Sheriff, A. (2001). Race and class in the politics of Zanzibar. *Africa Spectrum*. 36(3), 301-318.

Topan, F. (1971). *Mfalme Juha*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Traore, F. (2012). Family and society in Said Ahmed Mohamed's novels. *Swahili Forum*. 15, 73-75.

Wa Thiong'o, N. (1977). *Petals of Blood*. London: Heinemann.